# Kuimarisha **Utendaji wa Bunge** katika **Usimamizi wa Bajeti**

## Hoja ya Ofisi ya Bajeti ya Bunge.

### Hoja Husika

*Usimamizi wa Bunge uliohuru unahitaji pawepo na uhalisia wa kutenganisha na kuwa na uwiano mzuri wa mamlaka kati ya Bunge na Serikali. Pale ambapo hakuna mipaka na serikali ikiwa na nguvu kubwa kuliko bunge katika utoaji habari na rasilimali, achilia mbali kamati za usimamizi, haiwezekani kwa bunge kuwa na uwezo wa kuwa na makali endelevu dhidi ya serikali[1]. Kwa kuangalia utendaji wa Usimamizi wa Bajeti ya Bunge katika mazingira haya, hoja ya umuhimu wa kuanzisha Ofisi ya Bajeti ya Bunge inaweza kuibuliwa.*

*Ofisi ya Bajeti ya Bunge ni chombo huru kisichoegemea chama chochote cha siasa na kisichohusiana kabisa na serikali, ambacho kinatoa msaada wa kiuchambuzi kwa bunge na kusaidia utoaji wa maamuzi wakati wa kutathmini bajeti ya mwaka na mapendekezo mengine yanayowasilishwa na serikali kwa ajili ya kujadiliwa na bunge. Uibuaji wa mtazamo huu mpya utapelekea kuimarisha utendaji wa bunge katika usimamizi wa bajeti ambapo uwezekano wa kuwa na "bajeti mbadala" utakuwa mdogo au utakuwa haupo kabisa.*

### Utangulizi

Bunge linalo jukumu kubwa katika kuleta utawala wa kidemokrasia kwa kuhakikisha kuwa kuna uwazi na uwajibikaji toka serikalini. Utawala wa kidemokrasia unataka serikali iwe na uwezo, iwajibike, ishirikishe na iwe sikivu. Usimamizi wa bunge unachangia kwa sehemu kubwa katika suala hili kwa kushughulika na jukumu muhimu la kuwa na ufanisi katika kufuatilia na kupitia sera, utungaji sheria na uendeshaji wa serikali katika bajeti ya mwaka kwa niaba ya wananchi. Kwa kuzingatia usimamizi wa bajeti ya mwaka, kuifanyia kazi bajeti ya taifa, ndio njia sahihi ambayo kwayo mapendekezo yanayotokana na utendaji wa usimamizi wa bajeti ya bunge yanaweza kutekelezwa kiufasaha. Hata hivyo, ili suala hili liweze kutekelezwa, usimamizi wa bunge katika mchakato wa bajeti unapaswa kuwa wenye ufanisi au kuimarishwa kwa kusaidiwa na ofisi ya bajeti ya bunge.

Muhtasari huu unatoa mtazamo wa jumla wa utendaji wa bunge katika kutekeleza jukumu lake muhimu la kusimamia serikali, hususan usimamizi wa bajeti, na namna ambavyo jukumu hili linaweza kutekelezwa kwa kuanzishwa ofisi ya bajeti ya bunge.

### Uhalali wa Bunge kujihusisha na mchakato wa bajeti

Mchakato wa bajeti unapaswa kuwa sehemu muhimu ya utendaji wa bunge na wabunge. Hii ni kwasababu bajeti za serikali zinahusu kutenga rasilimali fedha za kutosha ambazo zinagusa maisha kwa viwango tofauti-tofauti vya wananchi ambao wanawakilishwa na wabunge katika taifa la kidemokrasia. Bajeti hujikita kwenye mwingiliano kati ya serikali na bunge katika kuuletea umma yafuatayo[2]:

(a) Taarifa juu ya miswada ya serikali;
(b) Ripoti za mahesabu, udhibiti wa fedha na utendaji wa serikali;
(c) Sheria na kanuni zinazotumika katika utengaji wa fedha; na
(d) Ripoti kamili katika mahesabu ya matumizi ya umma na usimamizi wa bunge.

Hata hivyo kwa Tanzania, kipimo cha serikali kuhusiana na ufanisi katika uwazi wa bajeti na usimamizi wa bunge bado kinaendelea kuwa chini. Bunge haliko mstari wa mbele kutekeleza jukumu katika upangaji wa bajeti na kusimamia michakato ya bajeti. Suala hili linabainishwa hapo chini katika sehemu ya "Kipimo cha serikali katika uwazi na usimamizi."

### Usimamizi wa Bunge katika Bajeti: *Mtazamo wa Jumla*

Usimamizi wa bunge unahusu uangalizi wa karibu katika shughuli za serikali na kuiwajibisha serikali kwa niaba ya wananchi kwa minajili ya kwamba ni serikali ambayo inatenga rasilimali kidogo kwa ajili ya wananchi[3]. Usimamizi wa bunge katika mchakato wa bajeti unajumuisha kufuatilia na kupitia upya mchakato mzima ikiwa pamoja na changamoto zote kwa upana wake ambazo serikali inakabiliana nazo, udhibiti wa matumizi na kupitisha bajeti ambazo zinaathiri matumizi ya sasa na ya baadaye. Kwa ujumla, utendaji wa usimamizi wa bajeti ni mojawapo ya mfumo wa kujipima ambao unahakikisha kuwa kuna uwajibikaji katika matumizi katika rasilimali fedha kidogo zilizopo.

Kwa Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingi zinazoendelea, utendaji wa usimamizi wa bunge kwenye bajeti unaonekana haufanyi kazi. Ushiriki wa bunge katika mchakato wa bajeti, huku ushiriki wa Kamati ya Fedha na Uchumi ukiwa mdogo, kwa sehemu kubwa ni utaratibu uliozoeleka wa kutia tu muhuri.

**HALI HALISI**

*Bunge la Tanzania halina mamlaka ya kubadili bajeti au kutenga fedha kwa ajili ya kazi zingine. Japokuwa Bunge laweza kukataa kupitisha bajeti inayowasilishwa na serikali, madhara ya hatua hii ni makubwa: Rais anayo mamlaka ya kikatiba ya kujibu mapigo kwa kulivunja bunge. Chanzo: Kuuelewa Mchakato wa Bajeti Tanzania, Mwongozo wa Asasi za Kiraia (2008) HakiElimu & Policy Forum*

Kwa sasa ushiriki mdogo wa bunge katika bajeti unajumuisha:

- Kupitia upya makadirio ya bajeti na kamati ya fedha na uchumi kwa kutumia taarifa kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi na idara zingine za serikali;
- Kutoa hoja ya kupitisha mapendekezo ya bajeti yanayowasilishwa na

Waziri wa Fedha na Uchumi katika kikao cha bunge;
- Kamati ya Fedha na Uchumi kuunga mkono hoja ya Waziri;
- Kikao cha kujadili bajeti ya taifa, na
- Kupitisha bajeti katika muda wa siku 40 kukiwa na marekebisho kidogo au yasiwepo kabisa.

Licha ya ushiriki huo, ufanisi wa mijadala ya bajeti unakwamishwa na sababu zilizoelezwa hapa chini.

Kwa ujumla wabunge huwa wanakosa uwezo katika umahiri wa maarifa ya kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika mchakato wa bajeti. Kwa sehemu fulani hali hii inatokana na ukweli kwamba wabunge wetu wana fani mbalimbali na historia tofauti katika masuala ya sheria, uhandisi, tiba, sayansi ya jamii, elimu, sanaa na mengineyo. Wakati baadhi yao wana utaalam, wengine hawana na wanakuwa wageni katika mchakato. Wabunge haohao huwa wanateuliwa kwenye kamati za bunge ambazo huwa zinakosa uwezo na utaalam wa kusaidia wabunge katika kuchambua sera jambo ambalo wanalihitaji ili kuimarisha usimamizi thabiti[4].

Aidha, upungufu huu huwa unadhoofishwa zaidi na desturi iliyozoeleka ya kukosa hamasa wakati wa vikao vya bajeti na mtazamo wa kwamba upangaji na uwasilishaji wa bajeti ni kazi ya serikali. Uthibitisho wa hili ni mahudhurio duni ya wabunge katika vikao vya kujadili bajeti ya sekta[5]. Matokeo yake ni kwamba, wakati wabunge wengine kwa ujumla wana uwezo wa kushiriki katika mijadala ya sera, lakini wanakuwa hawana uwezo wa kushiriki kikamilifu dhidi ya serikali katika masuala ya bajeti.

Ukosefu wa taarifa za kutosha kwa ajili ya kufanya uchambuzi yakinifu, pia ni kikwazo katika ushiriki mzuri wa wabunge kwenye mchakato wa bajeti. Wabunge wana udhaifu katika suala hili labda hadi pale ambapo sera inayojadiliwa iwe inahusiana na utaalam wao[6]. Hata kwa taarifa wanazopata, bado huwa hawana muda wa kutosha wa kuelewa na kujenga hoja nzito kwa ajili ya mjadala. Kazi inabakia kwa serikali kuwaridhisha wabunge na taarifa za dakika za mwisho, kiasi ambacho hujikuta wanaridhia sera si kwa kukubaliana nazo bali wanakuwa hawajui. Kinachofuata baada ya hapo ni ile desturi iliyozoeleka ya kuweka tu muhuri kama ilivyo kwa vikao vingine vyote vya bajeti.
Kwa kuongezea hapo juu, ni ule mtazamo mbaya wa kwamba jukumu la kusimamia serikali aghalabu huonekana kama ni wa vyama vya upinzani pekee, kwamba ndivyo vimeundwa kusimamia na kuanika ufisadi na utawala mbovu[7]. Hii ni kwasababu kwa sehemu kubwa ya bunge imegawanyika kivyama – huku chama tawala kikiwa na uwakilishi mkubwa na mpana. Wabunge wa chama kinachotawala ni nadra kuunga mkono hoja zilizoibuliwa na upande wa upinzani bila kujali kama watakuwa wako sahihi kuhalalisha upande wa serikali.

Mbali na hayo hapo juu, mabadiliko yanayohusiana na bajeti yamelenga tu serikali na michakato inayotokea huko. Mabadiliko mazuri ya bajeti, uwajibikaji kwa ujumla, matumizi na mifumo ya udhibiti na mipango mingine ya mabadiliko ndani ya bajeti yenyewe, yamelenga tu serikali – huku yakiacha mchango mkubwa ambao bunge lingetoa.

Zifuatazo ni baadhi ya sababu ambazo zinapelekea uchambuzi yakinifu wa usimamizi wa bunge katika bajeti usionekane kutokea.

## Kipimo cha serikali katika uwazi wa bajeti na usimamizi

Kipimo cha Tanzania katika tafiti za wazi za bajeti za 2006, 2008 na 2010, kimekuwa kikiendelea kuwa chini. Mpango Shirikishi wa Bajeti Kimataifa (International Budget Partnership), Utafiti wa Wazi wa Bajeti, ambako ndiko kipimo kilikonukuliwa; ni uchambuzi wa kina na utafiti ambao unatathmini iwapo serikali kuu zinatoa fursa kwa umma kupata taarifa za bajeti na kushiriki katika mchakato wa bajeti katika nchi zipatazo 85. Tanzania ilipata alama zifuatazo: 48%, 35% na 45% katika tafiti za miaka ya mtawalia 2006, 2008 na 2010, na kuwa moja ya nchi chache ambazo hutoa sehemu tu ya taarifa za bajeti ya serikali na shughuli za kifedha wakati wa kipindi cha bajeti. Utafiti huo pia unatathmini uwezo wa mabunge kuziwajibisha serikali zao.
Kwa kipimo cha bajeti ya wazi cha 2010, usimamizi wa bunge katika bajeti ulikuwa dhaifu kwasababu:
- Bunge halina mamlaka kamili ya kubadili mapendekezo ya bajeti ya serikali katika mwanzo wa bajeti ya mwaka;
- Bunge halina muda wa kutosha kujadili na kupitisha mapendekezo ya bajeti – huku ikipokea bajeti chini ya majuma sita kabla ya kuanza mwaka wa fedha; na
- Bunge haliendeshi mijadala ya wazi ambapo wananchi wangeweza kushiriki.

Katika nia njema ya utawala bora, ipo haja ya serikali kuboresha usimamizi wa bunge katika mchakato wa bajeti na kulifanya bunge kushiriki zaidi katika mzunguko mzima wa bajeti. Kuboresha ushiriki wa bunge katika mchakato wa bajeti kunaongeza usimamizi wa bunge kwa kuleta kichocheo cha kuyatumia mamlaka dhidi ya serikali huku ikiimarisha uwezo wake kiutaalam. Katika hoja yetu, kuimarisha usimamizi wa bunge katika bunge kunahitaji mabadiliko yanayolenga kutia nguvu utendaji wa bunge katika kusimamia mchakato wa bajeti. Mabadiliko ya bajeti, miongoni mwa mengine, yaliyotokea Nigeria, Ghana, Afrika Kusini, Kenya na Uganda yamefufua utendaji wa bunge katika kusimamia mchakato wa bajeti kwa kuunda chombo huru ndani ya bunge, ambacho kinachambua rasimu ya mapendekezo ya bajeti yanayotolewa na serikali na kutoa uchambuzi wa kina kwa wabunge ili kuwa na mapendekezo ya bajeti mbadala. Chombo kinachosemwa kinaitwa Ofisi ya Bajeti ya Bunge.

## Ofisi ya Bajeti ya Bunge ni nini?

Ofisi ya Bajeti ya Bunge (Parliamentary Budget Office - PBO) ni chombo huru kisichoegemea chama chochote cha siasa ndani ya bunge ambacho kinachambua rasimu ya bajeti iliyopendekezwa na serikali na inatoa msaada wa kiuchambuzi kwa wabunge ili waweze kuihoji hiyo rasimu na kuwawezesha kupendekeza bajeti mbadala[8]. Lengo lake kuu ni kutoa bajeti yenye mwongozo, taarifa za mwaka wa fedha na mipango kwa ajili ya wabunge ili waweze kuchangia, kutafsiri, kupitia upya na kutoa maamuzi mazito kuhusu mapendekezo ya bajeti – na kwa kufanya hivyo, wanatekeleza majukumu yao. Uhalali wa kuanzisha hii ofisi maalum unatokana na ukweli kwamba wabunge wanahitaji chanzo hiki cha taarifa na uchambuzi ambacho ni huru mbali na serikali ili kiweze kufanya kazi ya usimamizi wa bajeti kikamilifu[9].

Kuanzishwa kwa kitengo hiki ndani ya bunge kutawasaidia wabunge katika kuelewa mchakato wa bajeti, kujua changamoto zinazoikabili serikali kwa upana wake, kudhibiti

matumizi na kupitisha bajeti inayogusa matumizi ya sasa na yajayo. Kufanikiwa kwa utendaji wa ofisi hii kutapelekea kuboresha utawala bora kwa kusaidia kupanua zaidi uwazi na uwajibikaji na kuimarisha uwezo wa kitaalam wa wabunge katika kujadiliana na serikali kuhusu bajeti.

## Majukumu ya Ofisi ya Bajeti

Majukumu ya msingi ya ofisi ya bajeti ni[10]:

1. kutayarisha mapendekezo ya kiuchumi ambayo hayatokani na serikali
2. kutayarisha msingi wa makadirio ya mapato na matumizi
3. kuchambua mapendekezo ya bajeti yanayowasilishwa na serikali
4. kuandaa mapendekezo ya bajeti
5. kuchambua mapendekezo ya miradi mipya

Majukumu mengine ambayo pia yanaweza kufanywa na Ofisi ya Bajeti ya Bunge ni[11]:

- Kuangalia gharama zenye tija kwa mapendekezo yote mawili ya serikali na bunge,
- Kuandaa upunguzaji matumizi kwa mtazamo wa bunge,
- Kuchambua gharama za kanuni na mamlaka ya serikali za mtaa,
- Kufanya uchambuzi wa kiuchumi wa kina na wa muda mrefu,
- Kuchambua ufanisi wa sera za kodi zilizopendekezwa, na
- Kutoa mihtasari ya sera ambayo inaelezea mapendekezo na dhana za bajeti ambazo ni ngumu.

Machapisho kutoka Ofisi ya Bajeti ya Bunge hayana budi kuufikia umma, vyombo vya habari, asasi za kiraia, makundi yenye maslahi na raia – ambao serikali inawajibika kwao.

## Utofauti na Kamati za Bunge

Ofisi za bajeti zinatofautiana na kamati za bunge kama ifuatavyo[12]:

- Kazi za kamati zinajikita katika masuala ambayo zinaelekezwa na bunge.
- Kamati mara nyingi zina uhusiano na vyama vya siasa kwasababu zinaundwa na wabunge wanaotokana na vyama badala ya wachambuzi wenye mtazamo huru.
- Ofisi za bajeti kimsingi zinabobea katika uchambuzi wa fedha na bajeti ambao unachangia kupata bajeti na kuandaa makadirio ya bajeti yenye uwakilishi mpana tofauti na masuala ambayo kamati zinaweza kupewa mamlaka bila kujali kwamba mchango wake unasaidia bajeti au la.

## Uundwaji wa Ofisi ya Bajeti ya Bunge

Uanzishwaji wa Ofisi ya Bajeti ya Bunge yenye ufanisi, iliyo huru na isiyoegemea chama chochote cha siasa huhitaji kutiliwa maanani mambo yafuatayo[13]:

***Wafanyakazi:*** kwa kuzingatia uzito wa kazi ambayo Ofisi ya Bajeti ya Bunge itakabiliana nayo, kimsingi ofisi inatakiwa kuwa na wafanyakazi wenye umahiri wa utumishi ambao angalau wana shahada ya uzamili katika uchumi, fedha, kodi, uchambuzi wa takwimu, utawala na sera, na wenye uelewa mpana wa masuala ya uchumi na bajeti ambayo yanaathiri bajeti ya nchi. Pia itaongeza thamani kubwa kama wafanyakazi hawa watapata mafunzo au uzoefu wa kutosha wa kazi baada ya kumaliza shahada zao. Wafanyakazi wa muda mfupi wanaweza pia kuchukuliwa ili kuwasaidia wafanyakazi walioajiriwa moja kwa moja pale majukumu yanapoongezeka. Ili kuimarisha kitengo hiki na kuwavutia wafanyakazi, viwango vya malipo vya wafanyakazi vinapaswa kuendana na mishahara wanayopewa wataalam wengine katika nyanja zingine.

***Mahali:*** Ofisi ya Bajeti ya Bunge itakuwa vema ikiwa ni kitengo cha ndani cha bunge. Ukaribu huu una faida ya ofisi kuweza kuitikia na kuwajibika kwa wakati katika kujibu maswali ya wabunge na kuwa kitengo kilichoanzishwa kusaidia bunge katika kuendesha shughuli za kuisimamia serikali.

***Ufadhili***: Ofisi ya bajeti ya Bunge itafanya kazi vizuri endapo itakuwa na rasilimali fedha za kutosha. Hii inatokana na uzito wa kazi ambazo kitengo hiki kitakuwa nazo. Hii inatokana na ukweli kuwa kazi zake zitakuwepo mwaka mzima ikijumuisha tafiti na ukusanyaji taarifa, na ukweli kwamba ofisi hii itatakiwa kuwa na vifaa vya kutosha vya ofisi kwa ajili ya kuendeshea shughuli za kila siku ofisini.

***Uanzishwaji Kisheria***: Ofisi ya Bajeti ya Bunge inapaswa kujitegemea, na kazi zake za msingi inabidi ziwepo kisheria ili isije ikafungwa au kubadilishwa ili kukidhi malengo ya kisiasa. Sheria hiyo pia haina budi kufanya kazi katika kuisaidia Ofisi ya Bajeti ya Bunge kupata taarifa kwa kuilazimisha serikali kutoa taarifa za bajeti kwenye bunge kwa wakati. Kwa kuongezea, utungaji sheria unapaswa pia kufanya mabadiliko makubwa ya bajeti yanayolenga kusisitiza umuhimu wa ofisi hii na kuimarisha majukumu ya bunge katika mchakato wa bajeti.

***Sifa za kutoegemea chama cha siasa***: Ili Ofisi ya Bajeti ya Bunge iwe yenye ufanisi na tija, inapaswa kutoegemea chama chochote cha siasa katika shughuli zake, na wafanyakazi wanapaswa kuwa vivyo hivyo. Sheria ya kuanzisha Ofisi ya Bajeti ya Bunge inapaswa kusisitiza kuwa ofisi ihudumie vyama vyote katika bunge. Sifa hii itaifanya ofisi iweze kutoa taarifa sahihi kuliko kuwa na mlengo fulani wa kisiasa. Aidha inashauriwa kuwa, ili kuwa na uwiano, ofisi inapaswa kuhudumia kamati kuliko watu binafsi ambao wanaweza kuwa wanatafuta taarifa kwa maslahi yao.

***Majukumu ya Wabunge***: Kuwa na Ofisi ya Bajeti ya Bunge inayofanya kazi kwa ufanisi kunategemea utashi wa wabunge kuchukua jukumu la kushiriki katika upangaji wa bajeti na kutambua kwamba ofisi ya bajeti inachangia sehemu muhimu ya kuwasaidia kufanya majukumu yao. Wabunge, wakiwa wawakilishi wa watu, hawana budi kutambua kuwa wakitaka kuwajibika zaidi na kuwa na ufanisi katika kusimamia serikali, wajue kuwa bajeti ni mojawapo ya maeneo muhimu ambayo yanaweza kutoa ushawishi wao katika sera za maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

### Mfano wa ofisi ya bajeti inayofanya kazi: Ofisi ya Bajeti ya Uganda[14]

*Ofisi ya Bajeti ya Uganda ilianza kufanya kazi baada ya kutungwa Sheria ya Bajeti ya 2001. Imekuwa ikifanya kazi kwa ufanisi tangu ilipoanzishwa na imesaidia kuleta uwajibikaji kwa kuwezesha uchambuzi thabiti wa usimamizi wa bunge katika mchakato wa bajeti. Mojawapo ya majukumu inayoendelea kuyafanya ni:*

- *Ofisi ya Bajeti ya Bunge huwa inachambua taarifa za kila mwezi inazopelekewa na inatoa njia tofauti mbadala ambazo kwazo wigo wa kodi unaweza kupanuliwa. Imetoa ripoti ya kutambua maeneo muafaka ambamo upunguzaji wa kodi unachochea kuongezeka kwa watumiaji na kwahiyo kuleta mapato zaidi.*
- *Ofisi ya Bajeti ya Bunge inafuatilia ripoti za utoaji fedha kutoka kwa wafadhili ili kuweza kubaini kasoro*

*ambazo zitaifanya serikali iweze kubadili vipaumbele vya matumizi. Hali hii huboresha uwezo wa kamati kuweza kuelewa mikataba ya mikopo kati ya serikali na wafadhili. Bunge halipitishi tu mikataba kimazoea. Bunge sasa linakuwa na fursa ya kuitaka serikali kupitia upya vipengele ambavyo havina maslahi.*

- *Ofisi ya Bajeti ya Bunge inarekebisha upungufu uliopo na ufanisi wa bajeti nzima na inaleta dosari kwenye kamati ya sekta husika. Ofisi ya Bajeti ya Bunge inatoa ripoti ya ufanisi wa bajeti kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka ikizingatia taarifa iliyokusanywa kutoka hazina pamoja na sekta zingine. Hali hii hulifanya bunge kufuatilia utendaji wa bajeti nzima na ufanisi wa sekta maalum kwa mwaka mzima.*
- *Kwa kuwa Ofisi ya Bajeti ya Bunge inakuwa imeanzishwa, bunge linakuwa na uwezo kufuatilia taathira(matokeo) ya sera za uchumi mkubwa, linapokea taarifa huru kuhusiana na mwenendo wa umaskini na kuhakiki takwimu zinazotolewa na serikali kuhusiana na kukua kwa uchumi. Sasa, bunge linaweza kujadili katika uelewa, na inapobidi linaweza kupendekeza njia mbadala kwa serikali.*
- *Kwa masuala ambayo yanaendana na bajeti na uchumi, mwisho wa mwaka wa bajeti, Ofisi ya Bajeti ya Bunge nayo pia inatoa rekodi ya mapendekezo ya bunge kwa serikali ambayo kwayo inapaswa kushughulikia au kutekeleza – yakionesha wapi ambapo hayajatekeleza na sababu za kutoyatekeleza. Jambo hili linaweza kuimarisha usimamizi wa bunge kwa sehemu kubwa na kuboresha uwajibikaji wa serikali kwa bunge na hatimaye uwajibikaji wa wabunge kwenye majimbo yao.*

*Ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Ofisi ya Bajeti ya Bunge imeweza kufanikiwa katika mambo yafuatayo:*

1) *Kuondoa usiri wa mchakato wa bajeti. Mijadala ya wazi ya bajeti inakuwa ikifanywa ndani na nje ya bunge. Vikao vya kamati za bunge vinakuwa wazi kwa vyombo vya habari na umma, ambavyo vinafanya masuala yanayohusiana na bajeti kueleweka na wananchi wengi, na kwa ujumla kupanua wigo wa uwazi.*
2) *Ushiriki wa wabunge katika mchakato wa bajeti umeleta kukubalika kwa bajeti ikiwa pamoja na kuinua moyo wa kumiliki mchakato wa bajeti.*
3) *Sasa bunge linaweza kushughulikia matatizo kwa haraka kwa kuwa kuna mtiririko mkubwa wa taarifa na uchambuzi. Serikali inakuwa makini zaidi isifanye makosa katika utekelezaji.*
4) *Wafadhili wanakuwa na imani zaidi katika mchakato huu kuliko kabla ya hapo.*
5) *Kwa ujumla uwajibikaji unaongezeka. Kuchambua makadirio ya serikali kumeongeza uwajibikaji wake. Serikali inakuwa makini na mahiri katika kuandaa makadirio na kutoa ripoti. Kuna nidhamu kubwa katika kutumia fedha za umma kutokana na utendaji wa ofisi ya bajeti.*

*Muundo wa kitengo hiki wa kutoegemea chama chochote cha siasa umewezesha Ofisi ya Bajeti ya Bunge kufanya kazi kwa kiwango cha kuliridhisha bunge pamoja na serikali. Kitengo cha bajeti cha serikali sasa kinatambua na kukubaliana kwamba bunge linaweza kushughulikia masuala ya bajeti sambamba na serikali.*

## Hitimisho

Udhaifu wa utendaji wa bunge katika usimamizi wa bajeti huwa unaathiri uwajibikaji na utawala bora, ambao mwishowe huwa unaathiri jitihada zinazolenga maendeleo ya kiuchumi. Kwa mtazamo huu, hapana budi kwamba serikali irekebishe hali hii kwa kuimarisha utendaji wa usimamizi wa bunge katika mchakato wa bajeti. Thamani inayoongezeka katika utendaji wa usimamizi wa bunge kwa mchakato wa bajeti kutokana na utendaji wa ofisi ya bajeti ya bunge yenye ufanisi, isiyoegemea chama cha siasa na yenye dhamira safi, hauna mjadala.

Umefika wakati ambapo serikali inapaswa kutambua umuhimu wa bunge katika mchakato wa bajeti na sasa ianzishe ofisi ya bajeti ya bunge ambayo ni huru, isiyoegemea chama chochote cha siasa, ambayo inatoa msaada kwa bunge katika jukumu lake la kusimamia bajeti. Matokeo yake yatapelekea kuwepo uwajibikaji katika serikali ambayo nayo italeta matokeo mazuri katika maendeleo ya kiuchumi.

## Marejeo


***(Endnotes)***

1 Mwesiga Baregu, PARLIAMENTARY OVERSIGHT OF DEFENCE AND SECURITY IN TANZANIA'S MULTIPARTY PARLIAMENT, www.iss.co.za/pubs/Books/guardiansaug04/Baregu.pdf

2 The Report of a Commonwealth Parliamentary Association Workshop, Nairobi, Kenya, 10th -14th December, 2001, PARLIAMENTARY OVERSIGHT OF FINANCE AND THE BUDGETARY PROCESS, www.cpaafrica.org/.../Information.../Publications/...Publications/parliamentary%20oversight%20of%20finance%20and%20the%20b

3 Alan Hudson, ODI and Claire Wren, One World Trust, PARLIAMENTARY STRENGTHENING IN DEVELOPING COUNTRIES www.odi.org.uk/resources/download/103.pdf

4 Dr. Anthony Tsekpo (Parliamentary Centre) and Dr. Alan Hudson (ODI), PARLIAMENTARY STRENGTHENING AND THE PARIS PRINCIPLES TANZANIA CASE STUDY www.odi.org.uk/resources/download/3375.pdf

5 Evarist Kagaruki, An article entitled "ABSENTEE PARLIAMENTARIANS" in The Citizen Newspaper of Sunday 4th July, 2010 *(... as seen on TV as well*).

6 Dr. Anthony Tsekpo and Dr. Alan Hudson *op. cit.*

7 Hugh Corder, Saras Jagwanth, Fred Soltau, REPORT ON PARLIAMENTARY OVERSIGHT AND ACCOUNTABILITY, www.pmg.org.za/bills/oversight&account.htm

8 Jeffrey D. Straussman, Ari Renoni, ESTABLISHING A PARLIAMENTARY BUDGET OFFICE AS AN ELEMENT OF GOOD GOVERNANCE, www.cid.suny.edu/.../Straussman-Renoni%20CAP%20Note.pdf

9 Jeffrey D. Straussman, Ari Renoni *ibid.*

10 Jeffrey D. Straussman, Ari Renoni *ibid.*

11 John K. Johnson and Rick Stapenhurst, LEGISLATIVE BUDGET OFFICES: INTERNATIONAL EXPERIENCE, www.ndi.org/.../Legislative%20Oversight%20and%20Budgeting%20- %20Chapter%2010.pdf

12 Jeffrey D. Straussman, Ari Renoni *op. cit.*

13 John K. Johnson and Rick Stapenhurst *op. cit.*

14 Hon. Beatrice Birungi Kiraso, ESTABLISHMENT OF UGANDA'S PARLIAMENTARY BUDGET OFFICE AND PARLIAMENTARY BUDGET COMMITTEE, (*books.google.co.tz/books?isbn=082137611X*...)